Maswali

1. Ibrahimu alitaka Isaka aoe mke wa namna gani?
2. Ibrahimu alituma nani amtafutie Isaka mke?
3. Mbona Ibrahimu alituma Eliezeri amtafutie Isaka mke Harani?
4. Nani angemsaidia Eliezeri kupata mke mzuri?
5. Ni ishara gani Mungu angeonyesha Eliezeri mke aliyestahili?
6. Nani alitoka kwanza nje ya mji?
7. Rebeka alifanya nini kuonyesha kwamba Mungu alikuwa amemchagua?
8. Mbona Rebeka hakuogopa kuacha familia yake na kuenda kuishi mbali?
9. Rebeka aliona nani akija kondeni?
10. Mbona kulikuwa na furaha?

Majibu

1. Ibrahimu alitaka Isaka aoe mke anayempenda Mungu.
2. Ibrahimu alituma Eliezeri, mtumishi wake.
3. Ibrahimu alituma Eliezeri Harani kwa sababu watu wa familia yake wengine waliishi huko.
4. Mungu angeongoza Eliezeri apate mke aliyestahili.
5. Kwamba huyo mwanamke angempa maji anywe tena achotee ngamia zake pia.
6. Rebeka ndiye alitoka nje ya mji kwanza.
7. Rebeka alimpa Eliezeri maji akanywa, tena akawapa ngamia pia wakanywa.
8. Rebeka aliamini kwamba Mungu atamlinda.
9. Rebeka aliona Isaka kondeni akija.
10. Kulikuwa na furaha kwa sababu Isaka alikuwa amepata mke anayependa Mungu. Walioana na wote wakawa na furaha.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1

7 Mke wa Isaka

Kwa Biblia Mwanzo 24

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alijibu maombi ya Eliezeri. Kuonyesha kwamba ni maana kuoa mtu mlio na imani moja.

Somo

Wakati Isaka alikuwa mtu mzima, Ibrahimu alikuwa mzee sana. Isaka alikuwa mrithi wa ahadi za Mungu zote. Ibrahimu alijua ni la maana Isaka kuoa mke mzuri, mke anayempenda Mungu. Ibrahimu alimuita Eliezeri mtumishi wake wa maana. Ibrahimu alimwambia Eliezeri kwamba hataki mwanawe Isaka aoe mmoja wa wanawake Wakanaani, wasio mpenda Mungu. Ibrahimu alimtuma Eliezeri aende Harani. Familia ya Ibrahimu ingine ilikuwa inaishi huko. Ibrahimu aliambia Eliezeri amtafutie Isaka mke kutoka kwa familia yake huko Harani. Alimwambia Eliezeri kwamba Mungu atamsaidia kupatia Isaka mke mzuri. Eliezeri aliahidi kufanya juu chini ili apatie Isaka mke mzuri.

Mpango mkubwa uliandaliwa kwa safari ya Eliezeri. Isaka na Ibrahimu walichagua vitu vya dhamana vya fedha, dhahabu na nguo maridadi za kumpa bibi arusi pamoja na wazazi wake. Chakula kingi kilipebwa kwa ajili ya safari ndefu ya Harani. Eliezeri alianza safari. Alisafiri juu ya vilima, mabonde, akivuka majangwa na milima. Baadaye kwa umbali, akaona kuta za mji wa Harani.

Mapema jioni, Eliezeri alifika kwenye kisima nje ya kuta. Ilikuwa wakati wasichana walitoka kwenda kuchota maji kwa kisima. Eliezeri akaomba Mungu amsaidie apate mke mzuri wa Isaka. Akaomba Mungu aonyeshe ishara ya huyo mwanamke. Aliomba kwamba mwanamke atakayekubali akunyue maji kwa mtungi wake tena anyweshe ngamia zake maji ndiye atakayemchagulia Isaka.

Kabla Eliezeri amalize kuomba Mungu, maombi yake yalikuwa yamejibiwa. Msichana mrembo alitokea kutoka kwenye mji. Eliezeri alimkimbilia na kumwomba maji anywe. Alipoona kwamba ngamia nao walikuwa na kiu, alikimbia tena kuwachotea maji wanywe.



Eliezeri alimuuliza jina lake. Alikuwa Rebeka, mjukuu wa nduguye Ibrahimu. Eliezeri alishukuru Mungu kwa kumuonyesha mke mzuri wa Isaka – mmoja wa familia ya Ibrahimu. Eliezeri akampa Rebeka pete na vikuku vya dhahabu. Akamuuliza kama angekaa kwao kwa huo usiku. Rebeka alikimbia nyumbani kueleza familia yake yote yaliyotendeka huko mtoni. Walimkaribisha Eliezaeri akae nao kwao.

Eliezeri aliwambia sababu iliyomleta Harani. Aliwambia kwamba Ibrahimu alikuwa amekuwa na nguvu tena tajiri. Ibrahimu alitaka mwanawe Isaka aoe mke anayempenda Mungu.

Alikuwa amemtuma Eliezeri Harani ili amtafutie Isaka mke. Eliezeri aliwambia vile aliomba Mungu ili amwonyeshe mke anayestahili. Mungu alijibu maombi yake. Rebeka aliwapa ngamia maji na hiyo ilikuwa ishara aliyoiomba kutoka kwa Mungu.

Familia ya Rebeka waliposikia yote yaliyosemwa na Eliezeri, walijua kwamba Rebeka alikuwa amechaguliwa awe mke wa Isaka. Walikubali Rebeka asafiri na Eliezeri wakirudi ili amuoe Isaka.

Eliezeri alishukuru Mungu kwa kujibu maombi yake na kumchagulia Isaka mke mzuri. Eliezeri alimpa Rebeka na jamii yake vitu vizuri vya fedha, dhahabu pamoja na nguo maridadi sana.

Eliezeri alitaka kurudi upesi kwa Ibrahimu ili amuelezee habari njema. Walimuuliza Rebeka kama angependa kuondoka kesho yake asubuhi. Aliwajibu, “Nitaenda.” Rebeka alionyesha imani kubwa na kumtii Mungu. Alikubali kwenda safari ndefu kwa nchi geni na aolewe kwa mtu aliyekuwa hajamuona.

Kesho yake asubuhi mapema walianza safari. Rebeka aliaga familia yake. Alijua kwamba labda hawataonana tena kwa sababu alikuwa anaenda kuishi mbali sana. Rebeka hakuogopa. Alijua Mungu amembariki Ibrahimu, hata ameongoza Eliezeri kwa safari yake. Mungu alikuwa amechagua awe mke wa Isaka. Rebeka alijua Mungu atamlinda.

Baada ya kusafiri kwa mwendo mrefu, walikaribia alipoishi Ibrahimu. Jioni moja Rebeka aliona mtu akitembea kondeni. Yule mtu aliona ngamia na akaja kukutana nao. Rebeka aliuliza Eliezeri, “Ni nani huyu anakuja kukutana na sisi?” Eliezeri alijibu, “Ni bwana wangu Isaka.” Rebeka alishuka jini na kufunika uzo wake kwa shela.

Eliezeri alieleza Isaka vile kila kitu kilivyokuwa. Isaka alimchugua Rebeka kwa hema kubwa katikati ya kambi. Kulikuwa na furaha kuu. Isaka alikuwa amepata mke anayempenda Mungu. Isaka alimpenda Rebeka na akamuoa. Walikaa wote kwa furaha.